


I.25-

66



RAMAA PROPERTIES LIMITED

P. O. BOX 1556- KISASA NORTH, DSM RD, DODOMA.

PHONE: +255 715 427918; 758002401, +255 763 694394

E-mail: md@ramaa.com; info@ramaa.co.tz; website: www.ramaa.co.tz

Kumb: RAMAA/NIMRI/2019/07/001

Tarehe: 17 July, 2019

MKURUGENZI MTENDAJI,
TAASISI YA TAIFA YA UTAFITI WA MAGONJWA YA BINADAMU,
S.L.P 2448,
DAR ES SALAAM.

YAH: **KUTAMBULISHA MRADI WA VIWANJA ENEO LA MAPINDUZI 'A'
HALMASHAURI YA JIJI DODOMA.**


*QMS/DE
kindly scan and
email to all directors
and enter names
for stamp to NIMRI
Staffs.
Lumbi
18/7/19*

Tafadhali husika na Kichwa cha habari.

Kampuni ya **RAMAA PROPERTIES LIMITED** inayo heshima kutambulisha mradi wa viwanja vya matumizi mbalimbali katika eneo tajwa hapo juu. Mradi huu umekamilika katika kiwango cha viwanja kuidhinishwa na mamlaka husika kwa mauzo. Ukamilishaji huu ni pamoja na uchongaji wa barabara kufikia kila kiwanja. Mradi huu umefanywa kwa ubia kati ya kampuni yetu ya RAMAA PROPERTIES LTD na Halmashauri ya Jiji Dodoma.

Eneo la Mradi huu linazungukwa na maeneo nyeti kifursa kwa umbali tofauti. Maeneo haya ni Hospitali ya Benjamini/UDOM kwa upande wa Magahribi, Wizara ya Ulinzi na Ngome upande wa Kusini Mashariki, Mamlaka ya Bandari(Bandari Kavuu) na Stesheni ya Treni ya Kisasa/mwendo Kasi-Kaskazini; Stendi Mpya ya Mabasi, Soko Kuu jipya na eneo la Kujengwa Uwanja wa Kimataifa wa Michezo-Kaskazini Magharibi. Pia eneo hili linaunganishwa kwa barabara ya mzunguko wa Jiji na Mji wa Serikali upande wa Kaskazini.

Hivyo tunaomba kuwafahamisha na kuwakaribisha watu wote wenye uhitaji wa viwanja vya matumizi mbalimbali. Viwanja vimeandaliwa kukidhi mahitaji ya Makazi, Makazi na



Biashara, Biashara, Shule za awali, shule za Msingi na Sekondari. Pia kuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Hoteli, Masoko, 'Housing Estate', Nyumba za Ibada, Viwanda vya huduma/Kati na maeneo ya huduma za umma kama vile viwanja vya michezo, Makaburi, Viwanja vya Maegesho, Maeneo ya Wazi (Open Spaces) n.k.

Viwanja hivi vinauzwa katika halmashauri ya Jiji kwa kufuata taratibu zote za serikali kuanzia kujaza fomu ya maombi kwa gharama ya 20,000/ kwa kiwanja.

Kwa barua hii tunaomba nafasi ya kuja ofisini kwako kufanya uwasilishaji wa kina kuhusu mradi huu kwa wafanyakazi wa hapo Ofisi kwako ili wafanyakazi wako wapate nafasi ya kujua fursa zilizopo katika jiji la Dodoma ambalo ni Makao Makuu ya Nchi.

Ni matumaini yetu tutapata nafasi ya ushirikiano na Taasisi yako katika jambo hili.

Kwa mawasiliano zaidi unaweza kuwasiliana nasi kupitia simu zifuatazo:

+255 764 088 006
+255 763 761 914
+255 763 694 394

Wako katika ujenzi wa Taifa.



Innocent Fundisha

k.n.y **Mkurugenzi Mtendaji**